

## CHUO CHA MADINI DODOMA



### IDARA YA UHANDISI MIGODI NA UCHENJUAJI MADINI

#### KOZI YA MUDA MFUPI YA ULIPUAJI NA UCHORONGAJI MIAMBA (DRILLING AND BLASTING)

Chuo cha Madini Dodoma kimepewa mamlaka na Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini kufundisha Kozi ya muda mfupi ya Uchorongaji na Ulipuaji miamba kwa wote wanaohitaji kupata Cheti cha Kulipulia Miamba [**BLASTING CERTIFICATE (BC)**]

Mafunzo hayo yatawapatia Cheti cha Umahiri (**CERTIFICATE OF COMPETENCE**) ambacho kitamuwezesha muombaji kupata BC kwenye ofisi za Afisa Madini Wakazi (RMOs) Mkoa wowote Tanzania Bara.

Utaratibu wa mafunzo hayo ni kama ifuatavyo:

- i. Kwa wanaohitaji kuhuisha (renewal) BC zao watalipia **Tsh.150, 000.** (laki moja na hamsini elfu tu) kwa mtu mmoja kama mafunzo yao yatafanyikia chuoni (Dodoma au Nzega Kampas).

Na **Tsh.500,000.** (laki tano tu) Kwa mtu mmoja kama mafunzo hayo yatafanyikia eneo lake la kazi (***kwa wanafunzi wasiopungua kumi.***)

**Makundi haya yatapewa Mafunzo ya Muda Mfupi kwa muda siku MOJA mpaka TANO na kupewa mitihani maalum siku inayofuata.**

- ii. Kwa Wanafunzi wapya (wasiokuwa na BC) watalipia **Tsh.300, 000.** (laki tatu tu) kwa mtu mmoja kama mafunzo yao yatafanyikia chuoni (Dodoma au Nzega Kampas).

Na **Tsh.500,000.** (laki tano tu) Kwa mtu mmoja kama mafunzo yatafanyikia eneo lake la kazi (*kwa wanafunzi wasiopungua kumi*).

**Makundi haya yatapewa mafunzo ya muda mfupi kwa siku TANO mpaka KUMI kutegemea na uelewa wao na kupewa mitihani maalum baada ya kumaliza mafunzo.**

- iii. Kwa wale wenye Diploma (Stashahada) au Degree (Shahada) ya Uhandisi Migodi kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali wasiozidi mwaka mmoja tangu kuhitimu chuo

**Kundi hili Watapewa Mitihani Maalum tu kwa gharama ya Tsh.50, 000. (Elfu hamsini tu)**


### **NAMNA YA KULIPIA**

Ada ilipwe baada ya Mwanafunzi kuwasiliana na chuo na kupatiwa kumbukumbu namba (Control Number)

### **KWA MAWASILIANO ZAIDI**

Telephone No,	+255262300472
Mobile,	0713539890
	0765027403

Karibuni Saana



Joseph Mtui  
**Mratibu Mafunzo Mafupi**  
**09/10/2019**